

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO**



**DODOSO LA KUKUSANYA MAONI YA WADAU  
KUHUSU MAPENDEKEZO YA KUUNGANISHA BASATA, BODI YA FILAMU NA COSOTA**

1

**[WASANII]**

Kazi mbalimbali za Sanaa, ambazo ni sehemu ya tasnia ya ubunifu, zinakuwa na manufaa kwa mtendaji wa sanaa hiyo na kwa Taifa ikiwa zimelindwa ipasavyo chini ya misingi ya Hakimiliki na Hakishiriki. Kwa sasa masuala ya sanaa na Hakimiliki yanasiyamiwa na taasisi tatu tofauti ambazo ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (BFT) na Chama cha Hakimiliki (COSOTA).

Kwa Muda mrefu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo umekuwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji. Kwa mujibu wa wadau wa sanaa, baadhi ya changamaoto hizo ni mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi hizi, uwepo wa tozo zinazoingiliana pamoja na usumbufu unaotokana na taasisi zinazohudumia wasanii kuwekwa katika mamlaka tofauti kama vile Wizara ya HABARI, Wizara ya Viwanda na Biashara na TAMISEMI.

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali inakusudia kuunganisha taasisi hizo tatu na kuunda Mamlaka moja ambayo, pamoja na kuondoa kero kwa wasanii, itaongeza tija na manufaa kwa wahusika binfsi na Taifa kwa ujumla.

Kwa kuwa wewe ni msanii, unayo haki ya kushiriki katika kuboresha tasnia inayosimamia sanaa, kwa mantiki hiyo, unaombwa kujaza **dodoso hili ili tupate maoni yako muhimu** katika **historia ya Tasnia ya Ubunifu** na **Hakimiliki** nchini. Ni matumaini yetu kuwa maoni yako yataturufikia kuititia barua pepe zifuatazo: (1) [hglsu@habari.go.tz](mailto:hglsu@habari.go.tz) (2) [romanus.tairo@habari.go.tz](mailto:romanus.tairo@habari.go.tz) (3) [cosotatanzania@gmail.com](mailto:cosotatanzania@gmail.com) (4) [onesmo.ndinga@habari.go.tz](mailto:onesmo.ndinga@habari.go.tz). Tutaendelea kupokea majibu yenu kwa muda wa siku 14 tangu leo.

- (i) Jina la msanii.....
- .....
- (ii) Anuani ya Posta ..... Namba ya Simu .....
- (iii) Barua Pepe .....
- (iv) Aina ya Shughuli unayofanya katika tasnia hii;.....

Na.	HOJA	MAONI YA MDAU
1.	Ni taasisi gani kati ya zifuatazo inasimamia shughuli zako? (Weka tiki panapohusika). <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) BASATA</li> <li>(ii) COSOTA</li> <li>(iii) BODI YA FILAMU</li> <li>(iv) Taasisi nyingine (itaje)</li> </ul>	
2.	Serikali inakusudia kuuunganisha Taasisi za BASATA, BODI YA FILAMU na COSOTA ili kuunda Mamlaka	

	<p>moja ya usimamizi wa tasnia ya ubunifu na Hakimiliki nchini.</p> <p>Je unaafiki taasisi hizi ziunganishwe?</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) Ndiyo</li> <li>(ii) Hapana</li> </ul>	
3.	Kama jibu lako ni “Ndiyo” fafanua ni kwa nini, na pia kama jibu lako ni “hapana” fafanua ni kwa nini.	
2.	<p>Katika kuziunganisha Taasisi hizi, Serikali imependekeza kuunda taasisi moja itakayoitwa “Mamlaka ya Usimamizi wa Tasnia ya Ubunifu na Hakimiliki - <i>The Creative Industry and Copyright Management Authority (CICMA)</i>”</p> <p>Je, una maoni gani kuhusu jina linalopendekezwa?</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(a) Naafiki</li> <li>(b) Siafiki</li> <li>(c) Kama una maoni tofauti toa mapendekezo yako kuhusiana na jina la Mamlaka hiyo.</li> </ul>	
3.	Katika kuunganisha Taasisi hizi kutatokea mabadiliko katika muundo wa uongozi wa mamlaka pendekewa. Azma mojawapo ni kuwa na uongozi unaoshirikisha wasanii. Je una mapendekezo gani juu ya namna ya kuwapata wasanii watakaowakilisha wenzao kwenye uongozi wa mamlaka hiyo?	
4.	Pamoja na majukumu mengine, Taasisi inayopendekezwa itakuwa na jukumu la kuanzisha <b>Mfuko Mahsus</b> i kwa ajili ya kusaidia wahusika mbalimbali katika Tasnia ya Ubunifu na Hakimiliki nchini. Je, unapendekeza mambo gani yazingatiwe katika uanzishwaji wa mfuko huo?	
5.	<p>Taasisi inayopendekezwa inakusudiwa kuwa na mfumo mahususi wa utatuzi wa <b>migogoro</b> baina ya wasanii (wenyewe kwa wenyewe) na baina ya wasanii na wadau wengine wa sanaa au Mamlaka. Je unaafiki kuwepo kwa mfumo huo?</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(a) Ndiyo</li> <li>(b) Hapana</li> </ul> <p>Kama jibu ni hapana,</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(c) Je, una mapendekezo gani juu ya kuwa na mfumo bora wa utatuzi wa migogoro inayowahusu wasanii na wadau wengine wa tasnia hii?</li> </ul>	
6.	<p>Kwa kuzingatia umuhimu wa kutenda haki katika maamuzi ya Mamlaka inayopendekezwa, inakusudiwa kuwepo mfumo wa rufaa dhidi ya uamuzi uliotolewa na viongozi wa Mamlaka hiyo.</p> <p>(a) Je, Unapendekeza mfumo gani wa rufaa kati ya hii ifuatayo?</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi akate rufaa kwenda kwa Waziri,</li> <li>(ii) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi akate rufaa kwenda kwa Baraza la Ushindani wa Kibiashara (FCT),</li> <li>(iii) Mifumo yote kati ya (i) na (ii) itumike,</li> </ul>	

	(iv) Mahakamani. (b) Kwa nini unafikiri mfumo ulioupendekeza unafaa zaidi?	
7.	<p>Ili kusimamia utekelezaji wa masharti ya kisheria yatakayoainishwa katika Sheria ya Mamlaka inayopendekezwa kwa ajili ya kulinda haki za wasanii wa tasnia ya ubunifu na hakimiliki, inakusudiwa kuwepo kwa mfumo wa ukaguzi na uchunguzi (enforcement and compliance), utakaosaidia kufuatilia na kudhibiti vitendo vinyayohujumu kazi za wasanii na wadau wengine wa Sanaa nchini.</p> <p>(i) Je, unaafiki kuwepo kwa utaratibu huu? .....</p> <p>(ii) Ikiwa jibu lako ni hapana, Pendekeza njia unayofikiri inafaa ili kulinda haki za wasanii na wadau wengine wa tasnia.</p>	
8.	<p>Inakusudiwa kuwa Sheria itakayounda Mamlaka inayopendekezwa iweke utaratibu rahisi wa utoaji wa <b>leseni, vibali, vyeti au ithibati</b> kwa kazi mbalimbali za wasanii na wadau wa Tasnia ya Ubunifu na Hakimiliki.</p> <p>Je, ungependa mambo gani yazingatiwe wakati wa kuandaa mifumo au taratibu za utoaji wa hati hizo?</p>	
9.	<p>Serikali, kupitia Mamlaka inayopendekezwa, inakusudia kuunganisha huduma za tozo mbalimbali ambazo hutozwa na BASATA, Bodi ya Filamu na COSOTA ili zitolewe na taasisi moja tofauti na ilivyokuwa awali ambapo kila taasisi ilikuwa inatoza tozo hizo kwa mdau huyohuyo.</p> <p>(a) Je, ungependa mambo gani yazingatiwe wakati wa kutengeneza taratibu au mfumo wa tozo husika?</p> <p>(b) Unafikiri ni manufaa gani yatakayopatikana kutokana na kuunganisha tozo hizo?</p> <p>(c) Unafikiri ni changamoto gani zitatokana na kuunganishwa kwa tozo hizo?</p>	
10.	<p>Kuunganishwa kwa taasisi za Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu (BFT), na Hakimiliki na Hakishiriki (COSOTA) kutahusisha kuunganishwa kwa baadhi ya majukumu ya awali na kuibua mngine mapya kadiri ya itakavyopendekezwa na wasanii au wadau wengine wa Sanaa.</p> <p>(a) Je, unapendeleza mambo gani mapya yahusishwe katika usimamizi kwa ajili ya ustawi wa tasnia?</p> <p>(b) Je, ni faida gani mdau wa Sanaa au Hakimiliki atazipata kutokana na mambo hayo mapya?</p>	

[Endapo una maoni yanayozidi nafasi iliyowekwa kulia mwa kila swali, tumia nafasi iliyo nyuma ya kurasa hizi].